# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR




## SHERIA YA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII NAM. 3 YA 2018 KATIKA LUGHA NYEPESI ( KWA UPANDE WA KITAMBULISHIO CHA MZANZIBARI MKAAZI)

YALIYOMO…………………………………………………………………………………………………………
…i


DIBAJI ..................................................................................................................................... iv

UTANGULIZI............................................................................................................................... v

ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA ........................................................................................... vi

1.0 USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR............................................................................ 1

1.1 Nini maana ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar? ........................................... 1

1.2 Ni yepi matukio ya kijamii?........................................................................................................ 1

1.3 Matukio yanayotokea wapi yanapaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar? ........................................................................................................................... 1

1.4 Kuna aina ngapi za usajili wa matukio ya kijamii? ...................................................................... 1

2.0 USAJILI WA KADI YA UTAMBULISHO WA MZANZIBARI MKAAZI .................................................... 1

2.1 Nini maana ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?................................................................ 1

2.2 Kuna aina ngapi za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ......................................... 2

2.3 Ni upi utaratibu wa kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?............................................... 2

2.4 Ni zipi sifa za kupata kitabulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ......................................................... 2

2.5 Ni upi utaratibu wa kufuatwa ikiwa mwananchi hakuridhika na maamuzi ya Sheha katika kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? .......................................................................... 3

2.6 Ni zipi ada za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? .................................................. 3

2.7 Nini afanye mtu aliyepoteza kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?........................................... 3

2.8 Ni zipi athari za kutokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ......................................... 4

2.9 Je Kuna ukomo wa matumizi ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? .................................... 4

2.10 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ........................................................................................................................................ 4

2.11 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? .................... 4

2.12 Ni upi utaratibu wa kurekebisha taarifa katika kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ............... 5

2.13 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kukataliwa? ..................................................................................................................................... 5

2.14 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? ........................................................................................ 5

2.15 Ni yepi Makosa katika usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi? .................................... 6

3.1 Ni upi utaratibu wa usajili wa asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi? .................................................... 7

3.2 Ni zipi sifa za kupata kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi? ..................................... 7

3.3 Je Kuna ukomo wa matumizi ya kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi? .................... 7

3.4 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi? ......................................................................................................................... 7

3.5 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi ..... 8

3.6 Ni yepi Makosa katika usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi ...................... 8

## DIBAJI

Awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, mara tu baada ya kuingia madarakani pamoja na mambo mengine, iliagiza taasisi zake zinazotoa huduma kwa wananchi kutoa huduma zilizo bora na kwa wakati bila kuleta usumbufu kwa wananchi.

Vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahakikisha wananchi wote wanapata haki na fursa sawa bila kubagua kama inavyosisitizwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Uwepo wa misingi ya haki za binaadamu unabainisha kuwa pamoja na mambo mengine, haki ya msingi ya binaadamu baadaa ya kuzaliwa ni kupewa jina na kutambuliwa ili kurahisisha misingi ya upatikanaji wa haki.

Wakala wa Usajili wa Mtukio ya Kijaamii Zanzibar ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa rasmi chini ya Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018 kwa lengo la kusajili matukio ya kijamii yanayotokea Zanzibar. Matukio hayo ni pamoja na kizazi, kifo, ndoa, talaka na utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi.

Lengo la kufanya Sheria hii kuwa katika lugha nyepesi ni kuwasaidia wananchi wakiwemo wasimamizi, watumiaji na mawakala wengine waliomo kaktika kila Wilaya za Unguja na Pemba ili kuweza kuifahamu zaidi Sheria ya Wakala wa Usaji wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na utekelezaji wake.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa juhudi zao katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata uelewa wa Sheria, Kanuni na Miongozo yake katika kufanikisha suala la usajili wa matukio ya kijamii. Aidha, tunapenda kuwashukuru watendaji kutoka Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Jumuiya ya Center for Youth Dialogue (CYD) pamoja na Mradi wa Data Driven Advocacy (DDA) kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutayarisha Kitabu cha Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika lugha nyepesi.

Tunatoa wito kwa wananchi wote kukitumia Kitabu hiki kama nyenzo muhimu katika kutambua taratibu za usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar na kusajili matukio hayo kwa wakati.

## UTANGULIZI

Kitabu hiki cha ''Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar katika Lugha Nyepesi; Usajili wa Kadi ya Utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi'' kimetayarishwa ili kuwawezesha wananchi kuelewa kwa urahisi masuala yanayohusu taratibu ambazo mwananchi anapaswa kufuata pale anapohitaji kusajiliwa na kupatiwa kadi ya Uzanzibari Mkaazi. Kitabu hiki kimeweka wajibu kwa kila mtu anayehusika na suala la kutolewa kwa kadi ya utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi. Wajibu huu umeelezewa kwa kina na kufafanuliwa ili kila mhusika aweze kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria. Kuchapishwa kwa kitabu hiki, tunaamini masuala ya ''Usajili wa Kadi ya Utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi'' yatafahamika kwa urahisi zaidi na kila mwananchi.

Kitabu hiki kimefafanua utaratibu na hatua za kuchukuliwa na muombaji wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi pale anapohitaji kufanya maombi hayo ili aweze kupatiwa kitambulisho hicho. Aidha, ufafanuzi wa nani anayestahiki kupatiwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi umetolewa kwa kina kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018. Pamoja na taratibu hizo, Kitabu kinafafanua taratibu na sababu za kufutwa kwa usajili wa Mzanzibari Mkaazi, ili wananchi waweze kufahamu mazingira hayo yanayoweza kuwafanya kufutiwa usajili huo au kukataliwa maombi yao ya kusajiliwa na kupatiwa kitambulisho hicho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mbali ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kitabu hiki kimefafanua taratibu za usajili wa mtu asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi. Utaratibu huo unajumuisha uwasilishaji wa taarifa muhimu zinazohitajika ili kumsajili mtu kuwa asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi. Aidha, usajili huu pia unaweza kusitishwa kwa masharti yaliyotajwa kwa mujibu wa Sheria.

Masuala mbali mbali yanayohitaji kujulikana na wananchi yameelezwa kwa kutumia lugha rahisi katika kitabu hiki na mwananchi anaweza kufahamu kwa wepesi pale atakapokisoma. Kwa ujumla, Kitabu hiki kimetayarishwa kwa kuangalia vifungu vya Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2020 na kuviweka katika lugha ambayo inaweza kufahamika kwa urahisi na wananchi. Kwa namna kilivyotayarishwa, Kitabu hiki kinaweza kuwa msaada mkubwa kwa jamii katika kujenga ufahamu wa masuala ya utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi.

## ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA

- Katiba ya Zanzibar ya 1984
- Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya 2018, pamoja na Kanuni zake (Kanuni za za Usajili wa Matukio ya Kijamii 2020)
- Sheria ya Mzanzibari Nam. 5 ya 1985

## 1.0 USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

### 1.1 Nini maana ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar?

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, ni Ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa lengo la kusajili, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa vyeti vya matukio ya kijamii kama vile kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, cheti cha kuzaliwa, cheti cha kifo n.k (kifungu cha 3,4,21,27,35,39,43 Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 1.2 Ni yepi matukio ya kijamii?

Matukio ya kijamii ni:

i. kizazi;
ii. kifo;
iii. ndoa;
iv. talaka;
v. utambulisho wa ukaazi wa Zanzibar; na
vi. matukio mengine. (kifungu cha 2, Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 1.3 Matukio yanayotokea wapi yanapaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar?

Matukio yanayotokea ndani ya Zanzibar ndio yanayopaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

### 1.4 Kuna aina ngapi za usajili wa matukio ya kijamii?

Zipo aina mbili za usajili wa matukio ya kijamii ambazo ni:

i. Usajili wa matukio ya kijamii ndani ya wakati; na
ii. Usajili wa matukio ya kijamii nje ya wakati.

## 2.0 USAJILI WA KADI YA UTAMBULISHO WA MZANZIBARI MKAAZI

### 2.1 Nini maana ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

**Ni** kitambulisho cha ukaazi kinachotolewa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa lengo la kumtambulisha mtu kuwa yeye ni mkaazi wa Zanzibar, ambapo kitambulisho hicho hutolewa baada ya mtu kutimiza vigezo vilivyowekwa.

## 2.2 Kuna aina ngapi za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Kuna aina mbili za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ambazo ni usajili wa kitambulisho ndani ya wakati (kuanzia miaka 18-24) na usajili wa kitambulisho nje ya wakati (kuanzia miaka 25 na kuendelea).

## *2.3* Ni upi utaratibu wa kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Zipo aina mbili za taratibu za kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ambazo ni: -

- **Ndani ya wakati**

  Utaratibu za kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ndani ya wakati (kuanzia miaka 18 – 24) ni kwamba, Muombaji anatakiwa kuwasilisha vielelezo vifuatavyo katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iliyopo katika wilaya anayoishi: -

  i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa;
  ii. Nakala ya kitambulisho cha mzazi au mlezi kinachotambulika na Serikali;
  iii. barua ya uthibitisho wa ukaazi kutoka kwa Sheha; na
  iv. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 22 ya Kanuni za Wakala wa usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

- **Nje ya wakati**

  Utaratibu za kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi nje ya wakati (kuanzia miaka 25 na kuendelea) ni kwaamba, Muombaji anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ya kitambulisho katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar akiwa ameambatanisha na vielelezo vifuatavyo: -

  i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa;
  ii. Nakala ya kitambulisho cha mzazi au mlezi kinachotambulika na Serikali;
  iii. barua ya uthibitisho wa ukaazi kutoka kwa Sheha wa shehia anayoishi; na
  iv. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 23 ya Kanuni za Wakala wa usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

## 2.4 Ni zipi sifa za kupata kitabulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Sifa za kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni kama zifuatavyo**: -**

i. awe amezaliwa Zanzibar na ametimia umri wa miaka 18;
ii. awe ni raia wa Tanzania ambaye ameishi Zanzibar kwa muda wa miaka 10 mfululizo; na
iii. awe amekusudia kuendelea kuishi Zanzibar. (kifungu cha 4, Sheria Nam.5 ya 1985)

## 2.5 Ni upi utaratibu wa kufuatwa ikiwa mwananchi hakuridhika na maamuzi ya Sheha katika kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Iwapo mwananchi hakuridhika na maamuzi wa sheha katika kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi anatakiwa kupeleka lalamiko lake kwa Mkuu wa Wilaya, na ikiwa hakuridhika na uwamuzi wa Mkuu wa Wilaya anatakiwa kupeleka lalamiko lake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar. (Kanuni ya 24 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

## 2.6 Ni zipi ada za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Ufuatao ni mchanganuo wa ada za usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (Kanuni ya 23(3) ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

| S/N | KITAMBULISHO | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa muombaji asiyezidi miaka 25. | Bure (hakilipiwi) |
| 2. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa muombaji mwenye umri zaidi ya miaka 25. | TSH. 20,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kilichopotea kwa mara ya kwanza au kuharibika. | TSH. 20,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kinachohitaji marekebisho kwa mara ya pili. | TSH. 30,000/= |
| 5. | Kurekebisha taarifa katika kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. | TSH. 20,000/= |

## 2.7 Nini afanye mtu aliyepoteza kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Mtu aliyepoteza kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi atatakiwa kufika katika Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii iliyopo katika Wilaya anayoishi akiwa na barua ya Sheha pamaoja na barua ya Polisi yenye kuthibitisha kupotea kwa kitambulisho husika. (Kanuni ya 30 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

## *2.8* Ni zipi athari za kutokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

kutokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni kosa kwa mujibu wa sheria, kosa ambalo linapelekea athari zifuatazo: -

i. kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili na isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano (kifungu cha 53, Sheria Nam. 3 ya 2018);
ii. kukosa uthibitisho rasmi wa ukaazi wa Zanzibar;
iii. kukosa haki ya umiliki wa ardhi;
iv. kukosa ajira katika taasisi za Serikali;
v. kukosa haki za msingi kama vile kupiga kura, matumizi ya benki n.k.

## 2.9 Je Kuna ukomo wa matumizi ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Matumizi ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi yatasita iwapo kutatokea mambo yafuatayo**:**

i. kumaliza muda wa matumizi;
ii. kufariki kwa mtumiaji;
iii. kubadilisha uraia wa Tanzania; au
iv. kuwa na ukaazi wa kudumu nje ya Zanzibar.

## 2.10 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inaweza kufuta usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi endapo: -

i. itabainika taarifa za usajili sio sahihi;
ii. usajili umefanywa kwa njia ya udanganyifu, uongo au rushwa;
iii. kitambulisho kimetolewa kimakosa na kinahitajika kutolewa tena;
iv. usajili wa kitambulisho umefanyika zaidi ya mara moja; au
v. kuna Amri ya mahkama ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. (kifungu cha 49, Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.11 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi hufutwa kwa utaratibu ufuatao: -

i. kutolewa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi., taarifa hiyo hutolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na kupewa Muhusika wa kitambulisho hicho kinachotaka kufutwa;

ii. kupewa nafasi ya kujibu taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa muhusika;
iii. kufutwa kwa usajili wa kitambulisho hicho kwa kutolewa notisi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Muhusika; na
iv. kutoa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho hicho katika Gazeti Rasmi la Serikali.

## 2.12 Ni upi utaratibu wa kurekebisha taarifa katika kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Mtu anaweza kurekebisha taarifa katika kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa kuwasilisha barua ya maombi katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ikiwa imeambatanishwa na: -

i. hati ya kiapo kutoka Mahakamani au Kamishina wa Viapo;
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa cha muombaji; na
iii. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 40 ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

## 2.13 Ni sababu zipi zinazopelekea ombi la usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kukataliwa?

Ombi la usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi linaweza kukataliwa endapo: -

i. taarifa za muombaji sio sahihi;
ii. ombi halikufata utaratibu uliowekwa;
iii. ombi halikuambatanishwa na vielelezo muhimu vinavyohitajika;
iv. muombaji sio raia wa Tanzania; au
v. ikithibitika muombaji ana ukaazi wa kudumu nje ya Zanzibar.

## 2.14 Je kuna haki ya rufaa kwa asiyeridhika na maamuzi ya kukataliwa ombi la usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?

Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, ndani ya Siku 30 atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri anaehusika na usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar. (kifungu cha 21(7), Sheria Nam. 3 ya 2018)

## 2.15 Ni yepi Makosa katika usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi?


Mambo yafuatayo ni makosa kufanyika wakati wa maombi ya usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi:

i. kutoa taarifa za uongo;
ii. kumtumia mtu mwengine kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi;
iii. kutumia nyaraka zisizo halali;
iv. kumshawishi afisa msajili kufanya usajili kinyume na Sheria;
v. kwa uongo, kudai kupoteza au kuharibika kwa kitambulisho ili kupatiwa kitambulisho chengine;
vi. kunyang’anya au kuchukua kitambulisho cha mtu mwengine;
vii. kutumia kitambulisho cha mtu mwengine;
viii. kumiliki kitambulisho zaidi ya kimoja; au
ix. kumruhusu mtu kutumia kitambulisho cha mtu mwengine.

## 2.16 Ni zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu?

Adhabu za makosa yaliotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:
Faini isiyopungua shilingi za kitanzania Milioni moja na isiyozidi shilingi za kitanzania Milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili. (Kifungu cha 53(2), Sheria Nam. 3 ya 2018)

**Mfano wa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi**




## 3.0 Nini maana ya mtu asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi?

Mtu asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi ni mtu yeyote asiyekuwa mkaazi wa Zanzibar (Kifungu cha 2, Sheria Nam.3 ya 2018)

### 3.1 Ni upi utaratibu wa usajili wa asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi?

Utaratibu wa usajili wa asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi utafanyika baada ya muombaji kuwasilisha vielelezo vifuatavyo:

i. barua ya Sheha wa shehia anayoishi;
ii. Nakala ya kitambulisho cha Taifa au pasipoti ya nchi anayotoka;
iii. ruhusa ya kuishi au visa; na
iv. uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika.

### 3.2 Ni zipi sifa za kupata kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi?

Zifuatazo ni sifa za kupata kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi: -

i. Aliyekosa sifa ya kuwa Mzanzibari Mkaazi;
ii. Awe ametimiza umri wa miaka 18;
iii. Awe ameingia kihalali Zanzibar natanzania kwa ujumla;

### 3.3 Je Kuna ukomo wa matumizi ya kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi?

Matumizi ya kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi yatasita iwapo kutatokea mambo yafuatayo**:**

i. Kumaliza muda wa matumizi; au
ii. Kufariki kwa mtumiaji; au
iii. Kuwa na sifa za kupatiwa kitambulisho cha mzanzibari mkaazi; au
iv. Kumaliza muda wa matumizi ya kibali cha ruhusa ya kuishi zanzibar au tanzania kwa jumla.

### 3.4 Sababu zipi zinaweza kupelekea kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi?

Usajili wa kitambulisho cha asiyekuiwa Mzanzibari Mkaazi unaweza ukafutwa endapo:

i. itabainika taarifa za usajili sio sahihi;
ii. usajili umefanywa kwa njia ya udanganyifu, uongo au rushwa;
iii. kitambulisho kimetolewa kimakosa na kinahitajika kutolewa tena;
iv. usajili wa kitambulisho umefanyika zaidi ya mara moja; au
v. ikiwa kuna Amri ya mahkama ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi. (kifungu cha 49, Sheria Nam. 3 ya 2018)

### 3.5 Ni upi utaratibu wa kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi

Usajili wa kitambulisho cha asiyekuiwa Mzanzibari Mkaazi hufutwa kwa utaratibu ufuatao: - kutolewa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuiwa Mzanzibari Mkaazi, taarifa hiyo hutolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na kupewa Muhusika wa kitambulisho kinachotaka kufutwa;

i. kupewa nafasi ya kujibu taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulisho cha asiyekuiwa Mzanzibari Mkaazi kwa muhusika;
ii. kufutwa kwa usajili wa kitambulisho hicho kwa kutolewa notisi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Muhusika; na
iii. kutoa taarifa ya kufutwa kwa usajili wa kitambulissho hicho katika Gazeti Rasmi la Serikali.

### 3.6 Ni yepi Makosa katika usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi

Mambo yafuatayo ni makosa kufanyika katika usajili wa kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi:

i. kutoa taarifa za uongo;
ii. kumtumia mtu mwengine kupata kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi;
iii. kutumia nyaraka zisizo halali;
iv. kumshawishi afisa msajili kufanya usajili kinyume na Sheria;
v. kwa uongo, kudai kupoteza au kuharibika kwa kitambulisho ili kupatiwa kitambulisho chengine;
vi. kunyang’anya au kuchukua kitambulisho cha mtu mwengine;
vii. kutumia kitambulisho cha mtu mwengine;
viii. kumiliki kitambulisho zaidi ya kimoja; au
ix. kumruhusu mtu kutumia kitambulisho cha mtu mwengine.

### 3.7 Ni zipi adhabu za makosa yaliyoorodheshwa hapo juu?

Adhabu za makosa yaliotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:
Faini isiyopungua shilingi za kitanzania Milioni moja na isiyozidi shilingi za kitanzania Milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili. (Kifungu cha 53(2), Sheria Nam. 3 ya 2018)

CENTER FOR YOUTH
DIALOGUE